ARUSHA
FURSA LUKUKI

#Endless Opportunities

Toleo la Mtandaoni: 04 Tarehe 09/01/2023

#Kazi Iendelee

UTALII, KILIMO, BIASHARA NA UZALISHAJI

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN AKIZUNGUMZA NA VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA KUHUSIANA NA MAAMUZI YA SERIKALI YA KURUHUSU KUFANYIKA KWA MIKUTANO YA HADHARA KWA VYAMA HIVYO WAKATI WA KIKAO KILICHOFANYIKA IKULU JIJINI DAR ES SALAAM TAREHE 03 JANUARI, 2023.

ZAWADI ZA MHE. RAIS KWA WATOTO WALIOZALIWA KATIKA HOSPITALI YA MT. MERU ARUSHA.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Januari 1, 2023 ametoa zawadi ya kusherehekea Mwaka Mpya wa 2023 kwa Watoto waliozaliwa katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru pamoja na chakula cha mchana kwa Wagonjwa waliolazwa, Wagonjwa waliokuja kupatiwa matibabu, ndugu wa wagonjwa pamoja na watumishi wa Hospitali.

Akigawa zawadi hizo kwa niaba ya Mhe.Rais, Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John Mongella ameeleza kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha imechaguliwa kuwakilisha hospitali nyingine zilizomo Mkoani Arusha kuendesha zoezi hilo kama salamu ya heri ya mwaka mpya zilizotoka kwa Mhe.Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwatakiwa Wagonjwa wote uponyaji wa haraka pamoja na pongezi kwa Watoto waliozaliwa Hospitalini hapo.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Dkt. Frank Shega ametoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais kwa kuchagua hospitali ya Mount Meru kusherehekea pamoja kwenye Sikukuu hii ya kuukaribisha mwaka na kuongeza kuwa Wagonjwa wamefarijika kukumbukwa katika hali zao na wamemshukuru Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa moyo wa upendo aliouonyesha kwao na ametoa rai kwa Watu wengine kuiga mfano huo mzuri wa Rais.

Zawadi zilizotolewa ni pamoja na nguo za Watoto, track suti kwa Watoto, Blanketi, Shuka, Mafuta ya kujipaka, Pampasi, Sabuni za kufulia na kuogea, Chupa za Chai, Mwamvuli, Vitenge, Dawa za meno, Miswaki, Sukari, taulo za Watoto, n.k na Chakula cha mchana na vinywaji kwa Watu wote waliokuwepo Hospitalini.

MKUU WA MKOA WA ARUSHA ARIDHISHWA NA VIWANGO VYA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA MERU DC

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe.John Mongella amei-pongeza Halmashauri ya Meru kwa kukamilisha kwa wakati na ubora vyumba 17 vya madarasa katika Shule 13 za Sekondari wakati wa ziara yake ya kupokea vyumba vya madarasa Kim-koa.

Mhe.Mongella amesema Meru DC imekuwa ikitekele-za miradi yake kwa ubora wa viwango na kuwa hata vyumba hivyo alivyovikagua katika Shule ya Sekondari Muungano vimekamilishwa katika ubora unaotakiwa na kuwataka Viongozi ndani ya Mkoa Arusha kujituma na kushirikiana ili kufikia azma ya Serekali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ka-tika kuwaletea Wananchi Maendeleo. .

“ tunaona ufuatiliaji na ush-irikiano uliopo Meru kati ya Chama,Serikali na Wananchi mmefanya kazi kuwa nyepe-si “amesema Mhe.Mongella.

Mhe. John Mongella amese-ma uboreshaji wa Sekta ya Elimu unaofanywa na Serikali ya Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan,Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unalenga kutoa Elimu bora kwa kila mto-to wa kitanzania ambapo ameagiza Wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mwaka 2023 kuripoti mashuleni bila kuchelewa sambamba na Uongozi kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza darasa la awali na la kwaza wanaandikishwa.

Naye Mkurugenzi Mtenda-ji wa Meru DC Mwl.Zaina-bu Makwinya akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa amese-ma Halmashauri hiyo ili-pokea Milioni 340 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 17 vya madarasa pamoja na sama-ni zake (viti 50 na meza 50) katika Shule 13 za Sekondari ambapo amemshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani vyumba hivyo vitawanufaisha wana-funzi 6,938 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwan-za mwaka 2023.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha Mhe. Steven Zelothe Zelothe amempongeza Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mhandisi Richard Ruyango na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru kwa kutekeleza Ilani ya CCM inayolenga kuwaletea wananchi maendeleo kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Nao wazazi wameishukuru Serikali ya Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwani kwa sasa wamepungiziwa mzigo wa michango kwaajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na “tunafarijika kuona watoto watu wanasoma katika Mazingira mazuri kwani mbali na Serikali kujenga vyumba vya Madarasa imetoa fedha za viti na meza”amesema Samwel Kinga mkazi wa Usa-River.

Katika hafla hiyo fupi iliyo wa jumuisha Viongozi mbalimbali, Wananchi na Wanafunzi, Mkuu wa Mkoa wa Arusha amezindua vyumba viwili vya Madarasa katika Shule ya Sekondori Muungano ikiwa ni uzinduzi wa Vyumba vyote 17 vya Madarasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru .

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe.John Mongella akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoani Arusha katika Ibada ya Krismasi iliyofanyika katika Viwanja vya Shekhe Amri Abeid - Arusha

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akikabidhi zawadi za Krismasi kwa niaba ya Mhe, Rais katika kituo cha UMUAISHA Kata ya Osunyai Jijini Arusha.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akikabidhi zawadi za Krismasi kwa niaba ya Mhe, Rais katika kituo cha KINDNESS Kata ya Kimandolu Jijini Arusha.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akikabidhi zawadi za Krismasi kwa niaba ya Mhe, Rais katika kituo cha JOY OF GOD Kata ya Sekei Jijini Arusha.

VIONGOZI WA DINI MKOA WA ARUSHA WAMPONGEZA MHE. RAIS KWA KUKUZA DEMOKRASIA NCHINI.

Umoja wa Viongozi wa Dini Mkoa wa Arusha wamempongeza Rais Samia Hassan Suluhu kwa kuendeleza na kusimamia Demokrasia Nchini hususan kukwamua mchakato wa Katiba mpya na kuruhusu Vyama vya Siasa kufanya Mikutano ya hadhara.

Akisoma tamko la Umoja wa Viongozi wa dini Mkoa Arusha,Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa Dkt.Stanley Hotay alisema kuwa suala la kukwamua Katiba Mpya ni jambo la muhimu kwa Taifa.

Dkt,Hotay alisema katika kipindi cha Uongozi wa awamu ya nne,Serikali ilianzisha mchakato wa Katiba mpya, na kuwa Rais wa wakati huo aliunda Tume kwa ajili ya mchakato huo,

Tume hiyo ilifanya kazi ya kukusanya maoni ya wananchi lakini mchakato huo haukufikia mwisho.

“Tunapenda kuunga mkono hatua hii muhimu na adhimu liyochukuliwa na Rais Samia kufufua mchakato huu kwa manufaa ya Taifa hili.”
alisema

Pia alisema wamefurahi kusikia katika hatua za kufufua mchakato huo, wadau mbalimbali watahusishwa ili kuweza kupatikana kwa Katiba bora yenye kukidhi matakwa ya Watanzania.

Kuhusu mikutano ya hadhara kwa Vyama vya Siasa, alisema ni Vyema Vyama vyote vya Siasa vikafanya Siasa zao kistaarabu kwa kufuata sheria na miongozo mbalimbali inayosimamia sheria za Vyama vya Siasa ilikuepusha vurugu .

Aidha,Askofu Dkt.Hotay alisema Viongozi wa dini wanampongeza Rais Samia kwa kuendelea kutoa uhuru wa Vyombo vya Habari Nchini, kwani kuna uhusiano mkubwa kati ya uhuru wa Vyombo vya Habari na maendeleo ya Taifa lolote lile Duniani.

Alisema Rais alipoingia madarakani aliahidi kuvifungulia Vyombo vya Habari vilivyokuwa vimefungiwa na kweli Taifa na Dunia limeshuhudia akitimiza ahadi yake na kuvifungulia.

“Kwakuwa huu ni mwaka mpya, basi tufunge ukurasa uliopita kama Taifa na tufungue ukurasa mpya na tusamehane pale tulipokoseana. Tumepewa mwaka huu kwa Neema hivyo tuutumie vizuri kama Taifa.

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw. Missaile Musa pamoja na Afisa Elimu Mkoa Mwl. Abel Ntupwa [wa katikati] wakiwakabidhi Makubaliano ya Kimkataba Maafisa Elimu toka Halmashauri za Wilaya mara baada ya kikao kazi kilichofanyika Ofisini kwake.

NYUMBA YA WAGENI

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe.John V.K Mongella akiteta jambona Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi Mhe. Angeline Mabula alipowasili kwa ziara ya Kikazi Mkoani Arusha.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe.John V.K Mongella akiteta jambo na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima alipowasili kwa Ziara ya Kikazi.

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw.Missaile Musa akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Arusha, Lengo la Kikao hicho ni kujadili namna bora ya kuinua Sekta ya Michezo katika Mkoa wa Arusha.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw.Missaile Musa akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa Seksheni ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Mbadala toka Wizara ya Elimu na ```Mafunzo ya Amali Zanzibar.

OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TBS Prof. Othman Chande Othman, watatu kulia akiwa na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw. Missaile Musa wa tatu kutoka kushoto, pamoja na Wajumbe wa Bodi ya TBS ambao wapo Mkoani Arusha kwa Ziara ya Kikazi.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw. Missaile Musa akiwa Katika picha ya pamoja na Bi. Mashavu A. Shafih Mkurugenzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali toka SMZ